10 March, 2016

TAMKO KUHUSU NAMNA YA KUBORESHA UANDAAJI NA UPITISHAJI WA BAJETI YA SERIKALI

Tunatoa tamko hili sio kwa sababu hatujaona na kuthamini juhudu ambazo serikali ya awamu ya tano inafanya kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima bali tunakusudia kutoa tahadhari kwa watendaji wanaohusika na kutengeneza bajeti ya mwaka 2016/17.

Mapato ya serikali mara zote yamekuwa kidogo kuliko mahitaji yanayotakiwa kwa serikali kuweza kujiendesha, kutoa huduma na kuleta maendeleo. Kwa sababu hiyo serikali huwa inatengeneza mipango mikakati yenye vipaumbele vya matumizi ya mapato yake, na pale inaposhindikana inakopa na kuomba misaada kutoka kwa wafadhili.

Namna nyingine inayotumiwa na serikali katika kukabiliana na bajeti finyu ya serikali ni kukusanya mapato kikamilifu, kutumia rasilimali za umma kwa uadilifu, na kupunguza matumizi ya anasa na yasiyo ya lazima.

Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Mh. Rais John Pombe Magufuli imejikita katika kukusanya mapato ya serikali kikamilifu, kuongeza uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma, na kupunguza matumizi ya anasa na yasiyo na tija kwa jamii na taifa. Tunaipongeza serikali na hasa Mh. Rais kwa juhudi hizi.

Pamoja na kupongeza juhudi hizi za serikali, na kwa kuwa hiki ni kipindi cha kuandaa bajeti ya serikali ya mwaka 2016/17, tumeona vema kuwakumbusha watendaji kutokupanga mafungu makubwa kwenye matumizi ya anasa na yasiyo na tija. Tunaelewa kabisa kwamba matumizi yasiyo na tija huanzia mchakato wake kipindi hiki ambapo huwekwa kwenye bajeti na kisha baada ya kupitishwa na Bunge hutumika.

Kwa hiyo, tunatoa wito na angalizo katika yafuatayo; matumizi ya anasa na yasiyokuwa na tija, uandaaji wa bajeti usiozingatia vipaumbele na umakini na mchakato wa Bunge kupitisha bajeti ya serikali.

1. **Matumizi ya anasa na yasiyo na tija**

Tangu 2008, Sikika imekuwa ikifanya uchambuzi na kufuatilia bajeti ya serikali katika maeneo sita ambayo tunaamini yanavutia matumizi ya anasa na yasiyo ya lazima. Rejea machapisho kwenye tovuti yetu www.sikika.or.tz. Maeneo hayo ni katika **kulipa posho, mafunzo, safari, viburudisho, ununuzi wa magari, mafuta na vilainishi.**

Haya ni maeneo ambayo yamekuwa yakivutia matumizi makubwa ya fedha za umma licha ya serikali kuahidi bungeni kila mwaka kupitia hotuba ya Waziri wa Fedha kwamba wamepunguza matumizi hayo. Mfano, matumizi katika maneneo hayo sita yalikuwa shilingi bilioni 626.3 (2011/2012), shilingi bilioni 681.2 (2012/2013), (2013/2014) bilioni 714.1.

Tunatoa tahadhari lakini tunafahamu kwamba kuna posho na safari ambazo ni muhimu zifanyike. Kwa mfano, posho za madaktari na wauguzi (on call allowance) na safari zenye kuleta tija kwa taifa.

Mfano, Tanzania ilialikwa katika moja ya vikao vya Umoja wa Mataifa katika Tume ya Haki za Kiuchumi, Jamii na Utamaduni (United Nations Commitee for Economic, social and cultural rights) vilivyofanyika **Geneva, Uswiss** kuanzia tarehe 12-30 November 2012. Tanzania ilipeleka jopo la watu 34 ikiwa ni msafara mkubwa kuliko nchi nyingine zote zilizoalikwa, mfano Bulgaria (16), Ecuado (9), Iceland (6), Mauritania (13) na Equatorial Guinea (8). Pamoja na jopo hilo kutoka Tanzania kuongoza kwa ukubwa lakini wakati wa majadiliano katika kikao hicho watanzania walishindwa hata kujibu maswali. Kwa makadirio ya chini, ziara hiyo ilitumia zaidi ya shilingi milioni 400.

Taarifa hizi zimenukuliwa kutoka tovuti ya UN http://www2.ohchr.org/english/bodies...anzania_49.pdf na, Committee on Economic, Social and Cultural Rights - 49th session

2. Maeneo mengine yanayolalamikwa kwa matumizi mabaya ya fedha za umma

Ukiacha vipengele hivyo sita hapo juu yapo maeneo mengi yanayosababisha upotevu mkubwa wa fedha za umma, mfano; ununuzi wa kila mwaka wa samani (hasa kutoka nje ya nchi), ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kiofisi zaidi ya mahitaji na vyenye bei kubwa kuliko bei ya soko, sherehe mbalimbali za serikali, gharama kubwa za pango la ofisi, gharama kubwa za matengenezo na ukarabati (barabara, majengo na magari), mishahara hewa na uhamisho holela.

3. Uandaaji wa bajeti usio makini

Kwa miaka kadhaa Sikika imekuwa pia ikiangalia namna ambavyo bajeti ya mwaka ya serikali inavyoandaliwa na kuandikwa. Kwa ujumla serikali imekuwa ikijitahidi kuandika bajeti kwa kufuata miongozo na sheria husika. Lakini kuna maeneo machache ambayo yamekuwa sugu katika kukosewa wakati wa kuandika bajeti, kama ifuatavyo;

3.1 Kutumia kipimo tofauti kwa matumizi yanayofanana

Kuna maeneo ambayo matumizi yanayofanana yametengewa bajeti kwa kutumia vipimo tofauti. Mfano, malipo ya watu wanaosafiri (per diem) utakuta safari moja yamekadiriwa kwa kutumia idadi ya siku, safari nyingine yanakadiriwa kwa kutumia idadi ya watu, na safari nyingine yanakadiriwa kwa idadi ya miezi.

Mfano mwingine, unaweza kukuta kipimo kilichotumika kupanga bajeti ya mafuta ya magari ni lita au miezi. Tutakumbuka ripoti ya Bunge ya 2011 kuhusu kashfa ya Jairo, iliripotiwa kwamba magari yalitumia mafuta mengi kwa siku kuliko umbali yaliyokuwa yamesafiri, na wahusika walijilipa posho viwango tofauti kwa kazi moja.

3.2 Bei tufauti ya bidhaa au huduma moja

Ukikagua MTEF za baadhi ya wizara za serikali utagundua bei tofauti katika bidhaa au huduma inayofanana. Mfano unaweza kukuta sehemu moja dizeli imepangwa kununuliwa kwa bei ya lita moja Ths 2,200/ na sehemu nyingine ikatumika Tshs 3,000/

3.3 Bajeti isiyolenga kutekeleza malengo

Mara zote bajeti ya serikali hutakiwa kutekeleza malengo mahususi na serikali imekuwa ikijitahidi kufanya hivyo. Lakini kuna maeneo machache ambapo shughuli zinazopangwa kutekelezwa hazifikii malengo mahsusi yaliyopangwa na serikali.

Mfano, kama lengo ni kupunguza vifo vya akina mama na watoto tukielekeza bajeti kwenye semina na safari kila mwaka, badala ya kutoa na kuimarisha huduma kwa kundi hili, hatutapunguza vifo. Tunafahamu baadhi ya mambo yanayochangia vifo vya akina mama wajawazito, kwa mfano, ukosefu wa dawa, upungufu wa wahudumu, usafiri wa rufaa, ukosefu wa mashine za vipimo, upungufu wa sehemu za kujifungulia, damu n.k. Bajeti ikielekezwa huko tutatatua tatizo.

4. Umuhimu wa Bunge kuchambua bajeti kabla ya kupitisha

Kwa ujumla Bunge limekuwa likitimiza wajibu wake kukosoa na kupitisha bajeti za wizara na taasisi mbali mbali za serikali. Lakini Bunge linahitaji kuongezewa uwezo wake wa kuchambua bajeti ya serikali na kuirekebisha kabla ya kuipitisha.

Ili Bunge liweze kuichambua bajeti ya serikali ipasavyo, kamati zake zote zinatakiwa zipitie na kuchambua MTEF na siyo vitabu vikuu vya bajeti pekee. MTEF ndicho kitabu mama cha bajeti ya serikali kinachoainisha matumizi kwa kina. Vitabu vikuu vya bajeti, ambavyo wabunge wanagawiwa bungeni kwa ajili ya kupitisha haviwezi kuonesha kwa kina matatizo tuliyoainisha hapo juu.

Kwa kuwa wabunge wengi ni wapya ni muhimu serikali ikafanya mafunzo kwa wabunge kuwaelekeza muundo wa bajeti ya serikali ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Sambamba na hilo Bunge lianzishe na kuimarisha Ofisi yake ya Bajeti (Parliamentary Budget Office) iweze kuwasaidia wabunge kuchambua bajeti pamoja na kusaidia wananchi kupata taarifa mbali mbali za bajeti ya serikali

5. Bajeti iwekwe wazi mapema

Ili wabunge, wafanyabiashara, wanahabari, taasisi huru na wananchi waweze kuchambua na kutoa maoni yao kuhusu mwelekeo wa bajeti ya serikali ya mwaka 2016/17, ni muhimu vitabu vya bajeti na hasa MTEF za kila wizara na taasisi za umma zikawekwa wazi mapema iwezekanavyo. Bajeti za Mikoa na Wilaya zinatakiwa kuwekwa

wazi pia. Kwa upande wa wabunge, kanuni zinahitaji wapewe bajeti siku 21 kabla ya Bunge la bajeti kuanza. Tumeshuhudia miaka kadhaa wabunge wanapatiwa vitabu vya bajeti siku chache kabla ya vikao vya Bunge, kinyume na kanuni.

6. Badili muundo wa bajeti ya serikali

Wakati mwingine wizara, idara na halmashauri hulazimika kupanga fedha kwenye maeneo wasiyohitaji kwa sababu wanalazimika kufuata muundo wa bajeti waliopewa na Wizara ya Fedha. Badala ya Wizara ya Fedha kutoa muundo wa maeneo ya matumizi ya fedha za serikali, wizara na taasisi wangeachwa waamue wenyewe wanataka kutumia fedha katika maeneo gani na kwa namna gani kisha kuwasilisha Wizara ya Fedha

Kwa nini tunatoa angalizo muda huu?

Kwanza, tumekuwa tukitoa maangalizo kila mwaka isipokuwa sasa tunarudia kwa sababu tumefurahishwa na namna serikali iliyopo madarakani ilivyojipanga kudhibiti matumizi ili kuboresha huduma kwa wananchi. Hivyo tunayasema haya ili kuisaidia serikali kutimiza dhamira yake.

Pili, tunayasema haya kwa sababu serikali ipo katika hatua ya kutengeneza bajeti yake ya mwaka wa fedha 2016/17, na hivyo kutoa tahadhari ili bajeti inayoandaliwa iwe yenye vipaumbele na kuwa na matumizi yenye kuleta tija. Hivyo tunaiomba serikali ihakikishe inatengeneza bajeti yenye ufanisi na tija.

Tatu, tunayasema haya kwa sababu tuna Bunge jipya na hii ni bajeti yake ya kwanza. Tunaliomba Bunge kutimiza wajibu wake kikamilifu kuichambua bajeti kwa kupitia MTEF kwenye kamati zake za kudumu na kupeleka mapendekezo serikalini ili kuboresha bajeti kabla vitabu vikuu vya bajeti havijachapwa.

Mr. Irenei Kiria
Mkurugenzi Mtendaji wa Sikika,
P.O. Box 12183 Dar es Salaam,
Tel: +255 222 666355/57, Fax: 2668015, Email: info@sikika.or.tz, Website: www.sikika.or.tz